Umoja katika Mwili wa Kristo

“Kanisa ni mwili moja wenye viungo vingi, vilivyoitwa kutoka katika kila taifa, kabila, lugha na jamaa. Katika Kristo tu uumbaji mpya; tofauti za rangi, utamaduni, elimu na utaifa, na tofauti kati ya tabaka ya juu na ya chini, tajiri na maskini, mwanamume na mwanamke miongoni mwetu visitugawanye. Sisi sote ni sawa katika Kristo, ambaye kwa Roho mmoja, ametungamanisha katika ushirika mmoja pamoja Naye na sisi kwa sisi; yatupasa tutumike na kutumikiwa bila upendeleo au usetiri. Kupitia ufunuo wa Yesu Kristo katika Maandiko Matakatifu tunashiriki imani ile ile, na tumaini, na kuwafikia wote kwa ushuhuda mmoja. Umoja huu una chimbuko lake katika umoja wa Mungu mwenye nafsi tatu, ambaye ametufanya kuwa watoto wake.” (Rum.12:4, 5; 1Kor.12:12-14; Mt. 28:19, 20; Zab.133:1; 2Kor.5:16, 17; Mdo.17:26, 27; Gal. 3:27, 29; Kol.3:10-15; Efe.4:14-16; 4:1-6; Yoh.17:20-23)

Yesu baada ya kukamilisha jukumu lake duniani (Yoh.17:4) aliendelea kunyong’onyea kwa hali ya wanafunzi wake hata katika jioni ile kabla ya kusulubishwa. Wivu ulikuwa umetawala juu ya nani atakuwa na nafasi kubwa katika ufalme wa Kristo. Maelezo ya Yesu kwamba unyenyekevu ndio tunu kwenye ufalme wake yalionekana kuyafikia masikio yaliyoziba. (Luk.17:10). Hata kielelezo cha kuinama na kuosha miguu, hakikutosha kufikisha ujumbe. (Yoh.13:12-15). Yesu ni pendo na ndio maana alifuatwa na umati wa watu. Wanafunzi hawakuelewa jambo hilo na ndiyo maana waliwabagua wanawake, wasio Wayahudi, wenye dhambi na maskini. Ni upendo ndio unaomtambulisha Kristo na kututofautisha na ulimwengu (cf. Yoh.13:34, 35). Hata Getsemane, jambo kubwa lililomwelemea Yesu lilikuwa umoja wa Kanisa. (Yoh.17:21). Umoja ni zana isiyoshindwa ya kumshuhudia Yesu. (Yoh.17:23)

Umoja Kimaandiko na Kanisa

Hivi Kristo aliopoombea umoja, alikuwa na nia gani kwa ajili ya Kanisa linaloonekana leo? Huo upendo na umoja unawezekanaje? Misingi yake ni nini?

Umoja wa Roho. Roho Mtakatifu ndiye uwezo unaoshikilia umoja wa Kanisa. Kupitia kwake waumini wanavutwa kuingia Kanisani kwa kuwa wamebatizwa katika mwili moja. (1Kor.12:13). Waliobatizwa wapaswa kuwa na kile Paulo anachokiita umoja wa Roho. (Efe.4:3). Umoja huu ni wa mwili moja na Roho Moja kutokana na kumwamini Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, Mungu mmoja aliye Baba wa wote. (Efe.4:4-6).

Akiwaita watoke kwenye kila taifa na rangi, Roho Mtakatifu huwabatiza watu waingie katika mwili mmoja ambalo ndilo Kanisa.(cf.1Pet.2:5). Kila kanisa liko sawa, hata kama kuna makanisa yanayopokea misaada ya kiutume kutoka makanisa mengine.

Kanisa lenye umoja lina tumaini moja, “tumaini lenye baraka” ambalo litatimia katika “mafunuo ya utukufu wa Kristo, Mungu mkuu na Mwokozi wetu.” (Tit.2:13). Tumaini hili ni chanzo cha amani na furaha na hututia nguvu kuhubiri (Mt.24:14). Hutuongoza kubadilika kuwa watakatifu ili kufanana naye (1Yoh.3:3).

Kutokana na imani moja, imani ya mtu binafsi katika kifo cha Yesu kinalipia deni la dhambi, wote tunakuwa sehemu ya mwili moja. Ubatizo ambao huelezea kifo cha Yesu (Rum.6:3-6), huelezea vema ushuhuda wa umoja huu. Hatimaye Maandiko hufundisha kwamba yuko Roho mmoja, Bwana mmoja na Mungu mmoja ambaye ni Baba.

Mambo yote ya umoja hupatana katika Umoja katika Utatu Mtakatifu. Kwamba ziko karama tofauti, huduma tofauti, lakini ni kwa ajili ya Bwana yuleyule. Iko tofauti katika utendaji lakini ni Mungu azitendaye kazi zote katika wote. (1Kor.12:4-6).

Umoja hadi kufikia hatua gani? .Waumini hupitia uzoefu wa umoja wa kunia na kufanya maamuzi. Wanapaswa "kunia mamoja…na shauri moja" (Rum.15:5, 6; 1Kor.1:10). "Mkae kwa amani na Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi. (2Kor.13:11).

Umoja katika kutofautiana. Umoja wa kibiblia haumaanishi kufanana. Kwa kutumia mfano wa mwili wa mtu, ina maana umoja huwepo kwa kutofautiana. Mwili una viungo vingi lakini hufanya kazi tofauti, na hivyo, hakuna kiungo kisicho na kazi. Kanuni hiyo hutumika kanisani, Mungu anapogawa karama kadiri apendavyo. (1Kor.12:11). Ili kukamilisha utume, Kanisa lahitaji viungo vyake vyote. Yesu alitumia mfano wa mzabibu, kwamba Yeye ni mzabibu na wafuasi wake ni matawi. (Yoh.15:1-6). Kila tawi laweza ni mwendelezo wa mzabibu wa kweli, yaani Kristo. Zipo karama nyingi lakini Roho ni mmoja. Vile vile utendaji ni tofauti lakini ni Mungu yule yule atendaye kazi zote katika wote. (1Kor.12:6)

Umoja katika Imani. Kuwepo tofauti katika karama, haina maana kwamba kutakuwapo tofauti katika imani. Katika siku za mwisho, watakatifu wote watajulikana kwa kuwa washirika wa injili ya milele (Uf.12:6) wenye kuzishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu. (Uf.14:12).

Umoja unao umuhimu gani?
Pasipo umoja, kanisa halitaweza kuutimiza utume wake.

Umoja hufanya Juhudi ya Kanisa ifanikiwe. Katika ulimwengu uliovunjika kwa kutoridhika na migogoro, upendo na umoja wa washiriki wa kanisa wa aina tofauti, tabia tofauti na nafasi tofauti kwa vyeo, elimu na mali, hushuhudia ujumbe wa kanisa kuliko kitu chochote. Hili huonyesha muungano wao na mbinguni na kuthibitisha kwamba ni wanafunzi wa Kristo. (Yoh.13:35). Migogoro ya kikristo imefanya wasioamini watilie shaka ujumbe wa kikristo, na imekuwa kikwazo kikubwa kwa wao kuipokea injili. Umoja huvunja mtazamo huo. (Yoh.17:23)

Umoja hufunua Uhalisi wa ufalme wa Mungu. Kanisa lililoungana duniani huonyesha umakini wa wakristo katika matazamio yao ya kwenda kuishi pamoja mbinguni. Ufalme wa milele wa Mungu unafunuliwa na hutimiza maneno ya "Tazama jinsi ilivyo vema na kupendeza, ndugu wakae pamoja na kwa umoja." (Zab.133:1)

Umoja huonesha nguvu ya Kanisa. Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Kanisa huwa na ustawi na kuwa imara wakati washiriki wake wameungana na Kristo na wao kwa wao. Ndipo wanapokuwa watenda kazi pamoja na Mungu (1Kor.3:9).

Kuufikia Umoja

Chanzo cha umoja. Maandiko Matakatifu huonyesha kuwa umoja una chanzo katika (1) uwezo wa Baba Mungu, (Yoh.17:11); (2) Utukufu wa Baba ambao Yesu aliwapa wafuasi wake (Yoh.17:22); Kristo kukaa ndani ya waumini (Yoh.17:23). Roho Mtakatifu, Roho wa Kristo, ndiyo uwezo na kinachofanyisha kila kiungo kushikamana kwa umoja.

Roho Mtakatifu mwunganishi

Lengo ni umoja. Roho anapoingia kwa waumini, hufanya wapande juu dhidi ya mitazamo hasi ya tofauti za tamaduni, rangi, jinsia, utaifa na hadhi. (Gal.3:26-28).

Jukumu la karama za Roho kukamilisha umoja. "Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikilia umoja wa imani na kumfahamu sana

Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo na kimo cha utimilifu wa Kristo" (Efe.4:11-13). Tofauti ya karama zitakuza umoja wa Roho kuwa umoja wa imani (Efe.4:3, 13). Waumini wataimarika hata hawatadanganyika (Efe.4:14). Kupitia karama za Roho, waumini huusema ukweli kwa upendo na kukua katika Kristo, aliye kiongozi wa Kanisa. (Efe.4:16)

Msingi wa umoja

Ni kama Roho wa kweli (Yoh.15:26) Roho Mtakatifu atendaye kazi kutimiza ahadi ya Kristo. Jukumu lake ni kuongoza waumini katika kweli yote (Yoh.16:13). Kwa uwazi kinachofuatia ni kuwa, ukweli uliojengwa kwa Kristo ndio msingi wa umoja. Ni kweli kuwa ushirika, karama za roho, na upendo ni muhimu, lakini utimilifu wake huja kwa yule aliye kweli, na njia na uzima. (Yoh.14:6). Yesu aliomba uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndiyo kweli (Yoh.17:17). Kupata uzoefu wa umoja, waumini wapaswa kupokea nuru itokayo kwenye Neno. Ukweli huu ukikaa ndani, utawatakasa, kuwainua na kusafisha maisha, ukiondoa chuki na misuguano.

Amri Mpya ya Yesu. Kama mwanadamu, Kanisa limeumbwa kwa mfano wa na sura ya Mungu. Kristo aliagiza waumini wadhihirishe upendo wao kwa Mungu kwa kupendana wao kwa wao. (Mt.22:39). Kristo mwenyewe aliitii amri ya upendo kwa kipeo cha juu hadi Kalvari. Kabla ya kufa kwake aliagiza waumini wapendane, kama Yeye alivyotupenda. (Yoh.15:12 cf. Yoh.13:34).

Alikuwa kama anasema, "nawaagiza msisimamie haki zenu, kuona kwamba mnapokea mnachostahili, eti ikishindikana, mshitaki. Nawaagiza ninyi kuachia migongo wazi ili ichapwe, kugeuza shavu lenu mpigwe, kushtakiwa uwongo, kudhihakiwa, kukejeliwa, kuchubuliwa, kuvunjwavunjwa, kupigiliwa misumari kufa na kuzikwa, ikiwa kutenda hivyo, kutakuwa kuonyesha upendo wenu kwa wengine kama mimi nilivyofanya.

Kusikowezekana kunakowezekana. Je, twawezaje kupenda kama Kristo alivyopenda? Hili ni jambo lisilowezekana. Yesu anadai kisichowezekana. Hata hivyo ameahidi, Nami nikiinuliwa juu ya nchi nitawavuta wote kwangu (Yoh.12:32) Umoja katika mwili wa Kristo ni jambo lililotamkwa liwezekane. Una mizizi kwenye msalaba na kuchipua mioyoni mwa waumini.

Umoja katika msalaba. Tunapotambua kuwa pasipo Yeye hatuwezi kufanya lolote (Yoh.15:5), ndipo tunauona upendo wa Yesu kwa kuwa alikufa kwa ajili ya kila mtu pamoja na tofauti tulizonazo. Anatupenda sawa, yaani watu wa kila taifa, rangi, jamii na matabaka. Kalvari inamaanisha kuchukuliana mizigo (Gal.6:2). Alibeba mzigo wote wa mwanadamu uliovunja maisha Yake ili atupatie sisi uhai na kutuweka huru tupate kusaidiana.

Hatua za kufikia umoja. Umoja hauji moja moja. Yapaswa kupitia hatua kuufikia**.**

1. ***Umoja nyumbani***. Eneo muhimu kwa ajili ya kufundisha umoja ni kwenye familia. (Zab.133:1)

2. ***Kukusudia kuwa na umoja***. Hatutafikia umoja tusipoufanyia kazi kwa njia ya kuondoa tofauti kwa mazungumzo na kuuombea.

3. ***Kufanya kazi pamoja kufikia lengo la pamoja***. Kanisa halitafikia umoja hadi, likifanya kazi kama kikosi kimoja, kutangaza habari njema ya ufalme.(Mt.28:19). Twapaswa kuunganisha huduma ya kuponya na kuhubiri, kama Yesu alivyofanya. (Luk.9:2; 10:9).

4. ***Kuwa na mtazamo wa kiulimwengu***. Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi. Pasipo kutazama kanisa kiulimwengu, haiwezekani kufikia umoja.

5. ***Kuondoa mitazamo inayoleta mgawanyo***. Mitazamo ya kiubinafsi, kiburi, kujiamini, kujiona, chuki, kukosoa, kukemea and kutafutana makosa huchangia kudorora umoja wa kanisa. Mtazamo mpya wa Kalvari kutachipusha upendo wetu sisi kwa sisi (1Yoh.4:9-11). Paulo alitoa ushauri wa kutembea kwa roho (Gal.5:16) na kutembea huko huleta matunda ya roho ambayo ni dawa ya kufarakana. (Gal.5:22, 23). Yakobo alishauri kuepuka kupendeleana. (Yak. 2:9) hii ni kwa sababu Mungu hana upendeleo. (Mdo.10:34). Ni sawa kuheshimiana lakini kamwe tusione watu wengine kuwa wanapendwa zaidi na Mungu kuliko wenzao. (Mt.25:40). Kama Yesu kwa kuwa mwana wa Adamu alivyokuwa kaka kwa kila mtu, ndivyo alivyotutuma kwenda kuhubiri injili ya milele kwa kila taifa, lugha na jamaa.